


UKATAJI BORA WA SHINGO YA NDEGE



Utambuaji wa mishipa ya damu

Kuku



Bata Mzinga



Mishipa ya shingo inatumbulika kwa urahisi kwa sababu iko juu ya ngozi.

Halkumu iko ndani ya misuli ya shingo na **ndiyo mishipa muhimu zaidi ya damu kukata** kwa sababu inapeleka damu yenya oksijeni kwenye ubongo.


Katika kuku, bata bukini na kanga, halkumu zinaonekana kwenye misuli ya ngozi, karibu na kichwa.

Katika bata mizinga na mabata, mishipa imefichwa chini ya misuli kwa hivyo ni muhimu kukata misuli ili uione.


Ndege hizi hazijakatwa shingo lakini zimepasuliwa kuonyesha mishipa kamili ya damu

Matumizi

Mkato mlalo mkali kwenye misuli ya shingo, wa mbele ya shingo, kutoka upande mmoja hadi mwengine, chini mwa taya, unaitwa mkato ventrali wa shingo (VNC) na ni mbinu aminifu ya kukata **halkumu zote mbili za kawaida** na **mishipa yote miwili ya shingo ya nje**, katika spishi zote. VNC hufanya damu kuvuja **haraka**, kwa hivyo inapunguza mateso ya kuku na kuongeza ubora ya nyama.



Makadirio



Utirikaji wa damu ya **mishipa** wa umbo la V ya juu chini



Dalili za mkato unaofaa

Muda mfupi baada ya kukata shingo, kwa takriban sekunde 5 – 10, '**mitiririko**' **miwili miembamba ya damu** inafaa kufukiza kwa shinikizo la juu kwa umbo la V ya chini juu; hii inaonyesha kwamba **halkumu zote mbili za kawaida** zimekatwa.

- Wacha ndege ivuje damu kwa angalau dakika 2.25 – 3.
- langalie mara kwa mara kuhakikisha kwamba ndege haijapata fahamu.
- Thibitiisha ndege amekufa (ukosefu wa tendohiari endelevu na upumuaji) kabla ya kaendelea hatua zaidi.



Dalili za mkato usiofaa

Uvujaji pole pole wa damu au damu kutirikira mara moja baada ya mkato, hata kwa spishi ndogo (k.m. tomboo), inaweza kuonyesha vena zimekatwa lakini mishipa bado haujatengana. Kata shingo mara moja tena hadi uvujaji wa kutosha wa damu, au kata kichwa cha ndege.

Dokezo: hali fulani zinaweza kupunguza shinikizo la damu ya ndege (k.m. mapigo mepesi ya moyo; mshtuko wa moyo; utegukaji wa shingo; pistoli ya wanyama inaweza kusababisha uharibifu wa mishipa ya damu ndani ya kichwa) kwa hivyo huenda usione "mitiririko ya damu hata kama mishipa yote imekazwa.